Tume ya Kitaifa ya Kutetetea Haki za Kibinadamu nchini inasherehekea miaka mitatu tangu kubuniwa kwake mwaka 2003. Wengi watajiuliza Tume hii imeafikia nini katika kipindi hicho? Imeleta mabadiliko yapi kwa wakenya? Tunatumia fursa hi kuwaelezea wakenya yale ambayo Tumeafikia mbali na mikakati tulokumbana nayo katika kipindi cha miaka mitatu uliyopita. Hii siyo taarifa ya mwaka ya Tume hii. Kila mwaka Tume hii huchapisha ripoti inayoonyesha shughuli zake na matokeo. Ripoti hiyo ni ya mwaka 2003/4, 2004/5, na 2005/6.

Tume ya Kitaifa ya Kutetetea Haki za Kibinadamu ni kama asasi nyengine ile ya umma na ilibuniwa kupitia sheria ya kitaifa ya kutetetea haki za kibinadamu. Ilianza kutekeleza shughuli zake mnamo julai 29 mwaka 2003 wakati ambapo Rais kupitia mapendekezo ya bunge aliteua makamishna tisa kupitia mahojiano makali. Licha ya kubuniwa na serikali Tume hii ni huru. Shughuli zake huzingatia maafikiano ya *Paris* kuhusu asasi za kitaifa za kutetetea haki za kibinadamu yaliyoidhinishwa na Umoja wa Mataifa; na wala sio asasi ya namna yake inapofikia uhuru wake nchini na hata nyanja ya kimataifa. Jukumu la Tume hii ni kudumisha na kuhifadhi haki za kibinadamu. Tume hii ina majukumu mawili ya kimsingi; kwa upande mwingine ina jukumu la kulinda serikali. Inafuatilia mashirika ya serikali, inachunguza madai yoyote ya ukiukaji wa haki za kibinadamu na hata kutoa usaidizi kwa wale ambao haki zao zimekiukwa. Aidha, Tume hii ina jukumu la kutoa ushauri. Inatoa ushauri kwa serikali kuhusu namna ya kudumisha na kulinda haki za kibinadamu. Tume hii inaamini kuwa mashirika ya umma hayana budi kuwajibika kwa umma.

Kama mojawapo ya uwajibikaji, Tume ya Kitaifa ya Kutetetea Haki za Kibinadamu huchapisha kila mwaka kwa vyombo vya habari taarifa kuhusu yale iloafikia na mikakati yake mbali na kuandaa vikao kwa umma kuijadili na kuikosoa. Katika taarifa ya uwajibikaji ya mwaka huu, Tume hii imelenga yale ambayo imeafikia katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Mwaka huu vikao vya umma vya Tume hii vitafanyika katika maeneo matatu; Nairobi tarehe 19 Agosti 2006, Mandera tarehe 30 Agosti 2006, na Malindi katika taraha itakayotangazwa baadaye.

Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu inaongozwa na mikakati yake ya kipindi cha kati ya mwaka 2004 na 2009.

Mipango ya Tume hii inatekelezwa kutokana na mikakati mitano. Nayo ni:

- ↳ Upunguzaji wa ukiukaji wa haki za kibinadamu.
- ↳ Kuongoza katika harakati za hamasisho kuhusu haki za kibinadamu.

- ↪ Kuhakikisha mazingira ya ukuaji wa haki za kiuchumi, kijamii na tamaduni.
- ↪ Kubuniwa kwa mfumo bora wa elimu unaozingatia haki za kibinadamu.
- ↪ Kubuniwa kwa mashirika yenye uwezo wa kuhakikisha haki za kibinadamu.

Tume hii inatekeleza kazi zake kutokana na mipango ifuatayo.

- ↪ Mpango wa uchunguzi unachunguza ukiukaji wa haki za kibinadamu.
- ↪ Mpango wa urekebishaji unasimamia majukumu ya kisheria ya Tume hii ikiwemo kuhakikisha usaidizi kwa watu ambao haki zao zimekiukwa.
- ↪ Mpango wa kutoa mafunzo na hamasisho kuhusu haki za kibinadamu unashughulikia utoaji zaidi wa elimu kuhusu haki za kibinadamu kwa maafisa wa umma.
- ↪ Mpango wa sera na mafunzo unahusisha kuambatanisha masuala ya sheria katika udumishaji wa haki za kibinadamu.
- ↪ Mpango wa kampeni na utetezi unashughulika na polisi na mabadiliko katika sheria zinazotoa adhabu, haki na mikakati ya kupiga vita ufisadi.
- ↪ Mpango wa kuimarisha mashirika unasimamia raslimali za Tume hii na kuhakikisha mipango yake inaendelea sambamba.

Kama mashirika mengine ya umma, Tume hii imekua pakubwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Pamoja na mwenyekiti, kuna makamishna wengine wanane, wafanyikazi 30 na wanafunzi 22 wanaopata ujuzi wa kazi katika Tume hii.

Katika miaka mitatu iliyopita Tume hii imetumia shilingi milioni 51 kati ya mwaka 2003 na 2004, shilingi milioni 114 kati ya mwaka 2004 na 2005 na takriban shilingi milioni 200 kati ya mwaka 2005 na 2006. Makao makuu ya Tume hii yako Nairobi, na afisi ya kwanza ya kieneo ilifunguliwa Wajir katika Mkoa wa Kaskazini Mashariki mnamo tarehe 16 Juni 2006.

Kazi ya Tume hii haingefaulu pakubwa bila ya usaidizi wa makamishna, wafanyikazi, wateja wake, serikali, mashirika ya umma na washirika wa

maendeleo ikiwemo the Canadian International Development Agency, Australian International Development Agency, UNDP, National Endowment for Democracy, Action Aid, na wafadhili mbali mbali chini ya mpango wa mageuzi wa GJLOS.

Ili Tume hii iweze kuafikia majukumu yake ipasavyo serikali haina budi ila kuongeza ufadhili wake, kulinda uhuru wake mbali na kujitolea katika kuhakikisha mageuzi zaidi.

## 1. Kuishauri serikali kuhusu uingizaji wa haki za kibinadamu katika sera na sheria

Tumeishauri serikali kuhusiana na sera na sheria zilizopendekezwa katika harakati za kuhakikisha zinazingatia haki za kibinadamu. Mapendekezo kadhaa yameidhinishwa.

Kwa mfano:

- (a) Kutokana na uhakiki wa Tume hii pamoja na washirika wake, mswada kuhusu ugaidi wa mwaka 2003 ulitupiliwa mbali na serikali. Tume ya kitaifa ya kutetee haki za kibinadamu ilikuwa katika msitari wa mbele kupinga mswada huo kwa sababu ulionekana kukiuka haki za kibinadamu kwa sababu ulikuwa unamlimbikizia mshukiwa jukumu la kuthibitisha kwamba hakutekeleza kitendo cha ugaidi mbali na mengine mengi.
- (b) Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu ilishiriki pakubwa katika kuhakikisha uidhinishwaji haraka wa sheria za mahakama za kimataifa (ICC) mnamo machi mwaka 2005 na wakati huo huo ikashiriki kwenye harakati za kutaka sheria hizo za mahakama ya kimataifa kutumika humu nchini. Kutokana na ushauri wa Tume hii na wahusika wengine, serikali imepinga vikali shinikizo kutoka Marekani (USA) za kutaka sheria hizo kutotumiwa dhidi ya Wamarekani ambao huenda wakahusika na uhalifu wakiwa humu nchini maarufu kama ('Article 98' agreement).
- (c) Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu ilishiriki katika kuhakikisha mswada wa dhuluma za kimapenzi wa mwaka 2006 unapitishwa. Kutokana na ongezeko la visa vya dhuluma za kimapenzi humu nchini, Tume hii iliona haja ya kushiriki katika kampeni za kila aina kuhakikisha mswada huo unaidhinishwa. Kutokana na kupitishwa kwa mswada huo, Tume hii sasa inahisi watoto wa kike wa kiume pamoja na wanawake ambao wamejikuta katikati mwa dhuluma za kimapenzi watalindwa ipasavyo.
- (d) Serikali imeidhinisha mapendekezo ya Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu kuhusu marekebisho katika sheria ya ushahidi, hasa uwezo wa polisi kutwaa ushahidi kutoka kwa mshukiwa. Uwezo huo ulipokonywa polisi katika mabadiliko katika sheria ya ushahidi mwaka 2002, ambayo ilishurutisha ushahidi kutolewa mahakamani pekee. Polisi waliteta kuwa mabadiliko hayo yalititiza harakati zao za kupiga vita uhalifu kwani huenda hakimu asiwepo wakati ambapo mshukiwa anataka kuandikisha taaarifa yake. Mashirika ya

kutetea haki za kibinadamu yalihofia huenda zikarejea tena zile enzi ambapo polisi waliwatesa washukiwa wakati wakitwaa ushahidi. Tume hii ilimshauri Mkuu wa Sheria kuhakikisha mabadiiko katika sheria ya ushahidi yatakayoruhusu tu afisa wa polisi wa kiwango cha inspecta mkuu kutwaa ushahidi kutoka kwa mshukiwa lakini kuwepo mtu mwingine aliyechaguliwa na mshukiwa. Mapendekezo hayo yalikubalika. Yamo katika mswada wa mwaka 2006 (Miscellaneous Amendments).

Mapendekezo haya pia yanamtaka Mkuu wa Sheria kuwa na mashauriano na Chama cha Wanasheria Nchini, Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu na mashirika mengine yanayostahili, kubuni sheria zinazosimamia utoaji ungamo kwa polisi.

- (e) Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu ikishirikiana na Tume ya Kufanyia Marekebisha Sheria, Magereza na washikadau wengine imependekeza mabadiliko katika sheria na kanuni ya magereza. Makamu wa Rais, ambaye idara ya magereza iko chini yake alipokea vyema mapendekezo hayo. Tume hii ilishinikiza mabadiliko hayo katika harakati za kuhakikisha kutelezwa kwa haki za kibinadamu katika magereza. Kwenye mapendekezo yake, Tume hii ilitaka magereza kuwa maeneo ya kurekebisha tabia badala ya kuwa maeneo ya mateso kama mojawapo ya njia za kupunguza uhalifu nchini.
- (f) Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu imechangia katika kuhakikisha kukubalika kwa hali kuwa haki za kiuchumi na kijamii ziidhinishwe katika mswada wa sheria za haki za kibinadamu. Sasa kuidhinishwa kwa haki za kiuchumi na kijamii katika msada wa sheria za haki za kibinadamu sio swala bishi. Wakati wowote ule wakenya watakapoanza kuijadili katiba mpya kujumuishwa kwa haki hizo hakutapingwa. Tume hii ilichapisha mapendekezo kuelezea ni kwanini haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni zinahitaji kujumuishwa katika sheria za haki za kibinadamu.
- (g) Tume ilifanyia mabadiliko sheria kuhusu usimamizi wa raslimali za maji (mswada wa kwanza) katika mswada uliofanyiwa mabadiliko wa juni 2006 . Asilimia 60 ya mapendekezo ya Tume hii yameidhinishwa. Hii ilihusisha mipango kabambe ya maji, kuhakikisha maskini hawanyanyaswi na matajiri ama kampuni za kibinafsi za maji na kuhakikisha kuwa taarifa kuhusu maombi ya leseni za maji yanawasilishwa katika afisi za mabaraza ya miji ili kuwezesha jamii kuifikia rahisi.

- (h) Serikali imekubali mapendekezo kubuni sheria dhidi ya matamshi yanayozua uhasama na chuki. Waziri wa Sheria na Maswala ya Katiba amejitolea binafsi kuongoza katika uchapishaji na ubunifu wa sheria hizo ambazo zitawasilishwa bungeni. Tume ya kitaifa ya kuteteta haki za kibinadamu inaandaa mapendekezo yake.
- (i) Serikali imeidhinisha mapendekezo mengi ya Tume ya kitaifa ya kutetea haki za kibinadamu kuhusu hali ya haki za kibinadamu nchini yaliyo kwenye ripoti yake ya 2003/4. Ripoti hiyo ilithibitisha kuwa sera za serikali hazizingatii swala nyeti la usawa nchini, katika maeneo ya humu nchini, miongoni mwa makundi ya kijamii na makundi mengine. Mpango wa wizara ya afya unaonekana sasa kuzingatia swala la usawa kote nchini. Ripoti hiyo pia ilipendekeza kuwa ili viwango vya afya vidumishwe nchini, basi itabidi zahanati na vituo vya afya zaidi kujengwa ili kuhakikisha maskini wananufaika na vifaa vya afya. Hilo linaanza kudhihirika wazi.

Kuhusiana na maswala ya usawa, Tumeridhika kuwa ingawa neno hilo lilitajwa mara tatu pekee katika taarifa ya bajeti ya kati ya mwaka 2003 na 2004, na ile ya 2004 na 2005 maswala ya usawa yalitajwa mara 19 katika bajeti ya mwaka 2006 na 2007. Utoaji sawa wa raslimali umetambuliwa kama njia mwafaka ya kuhakikisha watu wanaotengwa katika jamii wanatengewa raslimali. Mfano ni vijana na wazazi wachanga.

Kuhusu elimu, ripoti hiyo ilionyesha kuwa taasisi za mafunzo anuwai zimetetekezwa kwa kutotengewa raslimali katika bajeti. Katika bajeti ya mwaka 2006 na 2007 pesa zimetengwa kupitia hazina ya ustawi wa maeneo bunge kufufua angalau taasisi moja ya mafunzo anuwai katika kila eneo bunge.

Mapendekezo kuhusu hali ya haki za kibinadamu nchini ya mwaka 2003 na 2004 yanashawishi namna washirika wa kimaendeleo humu nchini kama vile GTZ Kenya wanavyotoa misaada.

Tume hii, imefanyia marekebisho miswada mingine ambayo kwa sababu moja au nyingine haijakuwa sheria. Hii ni pamoja na mswada wa bima ya kitaifa ya matibabu wa mwaka 2004, mswada wa kulinda mashahidi wa mwaka 2005, mswada uliopendekezwa wa kahawa na ule wa uhuru wa vyombo vya habari.

## **2. Kuhakikisha uwajibikaji katika matumizi ya mali ya umma**

Tume hii, imachangia katika kuhakikisha serikali inawajibika kwenye matumizi ya mali ya umma, hali ambayo imepelekea kuokoa shilingi bilioni 1.5. Pesa hizi zinaweza kutumika kwenye miradi ya maendeleo kwa ajili ya watu maskini. Kutokana na kuchapishwa kwa taarifa ya Tume hii kwa kichwa; *'Living Large'* mnamo Februari mwaka 2006, ambayo ilionyesha ubadhirifu wa mali ya umma kupitia mawaziri na mawaziri wasaidizi kununuliwa magari ya kifahari, serikali ilichukua hatua mwafaka. Matumizi mabaya ya raslimali za umma hupelekea raslimali ndogo kutengewa maskini, huathiri ununuzi wa dawa za kukabiliana na makali ya ukimwi, hazina ya malipo ya elimu kwa watoto kutoka jamii maskini pamoja na hazina ya kukabiliana na baa la njaa. Ripoti hii ilichapishwa kwa pamoja na shirika la Transparency International (TI-Kenya).

Katika taarifa rasmi kwa makatibu wa wizara tarehe 31 Machi mwaka 2006, Mkuu wa Utumishi wa Umma na Katibu wa Baraza la Mawaziri aliwauliza Makatibu wa Wizara kuandaa taarifa kuhusu magari rasmi ya serikali yalotengewa mawaziri na mawaziri wasaidizi katika wizara zao na kuiwasilisha kwake.

Katika bajeti ya mwaka 2006 na 2007, waziri wa fedha aliidhinisha mapendekezo ya Tume hiyo kuhusu upunguzaji wa matumizi mabaya ya mali ya umma kupitia ununuzi wa magari. Waziri alipiga marufuku utumiaji wa magari ya umma kwa shughuli za kibinafsi. Katika kuhakiki swala hilo vyombo vya habari vilirejelea ule utafiti wa Tume hii kwa kichwa; *'Living Large'*. Waziri aliahidi kutwaa magari yote katika kipindi cha miezi miwili na kupendekeza mengi yao kuuzwa.

Tunatarajia kuwa serikali itaidhinisha kwa dhati sera hiyo. Serikali iliyotangulia ilikosa kutekeleza azimio kama hilo kutokana na kutokuweko nia ya kisiasa.

## **3. Kuhakikisha uwajibikaji katika shughuli za uchaguzi**

Wakati wa kampeni za kura ya maoni kuhusu katiba mpya mnamo Novemba mwaka 2005, Tume hii ilianzisha harakati za kuchunguza kampeni hizo ikizingatia hasa matumizi ya matamshi ya kuzua uhasama na chuki, uchochezi mbali na matumizi ya raslimali za umma kinyume na sheria.

Tume hii ilitoa orodha ya majina maarufu kama *list of shame* ambayo ilionyesha ni afisa yupi wa serikali aliyetumia raslimali za serikali na

wale waliotumia matamshi ya kuzua chuki na uhasama. Punde taarifa hii ilipochapishwa katika vyombo vya habari kulikuwa na mabadiliko katika mienendo ya maafisa wa serikali. Wengi walikomesha tabia ya matumizi ya raslimali za umma pamoja na lugha chochezi. Wale walioendelea kutumia raslimali za umma walidai kuwa wameilipia katika juhudi za kutaka kusafisha majina yao. Kulikuwa na ongezeko la matumizi ya magari yenye usajili wa magari ya kibinafsi licha ya kwamba yalikuwa ya umma.

Maafisa wengi wa serikali waliaibika pakubwa. Wakenya wakaanza kuripoti maafisa wa serikali wanaotumia magari ya umma, raslimali nyingine za umma, wenye matamshi ya kuzua chuki na wachochezi.

Tume hii, iliwasilisha kesi ya kibinafsi dhidi ya waziri msaidizi na Mbunge wa Hamisi George Khaniri, kwa uchochezi kinyume na kifungu 96 cha sheria. Aidha iliwasilisha kesi nyengine dhidi ya Mwenyekiti wa KENGEN Titus Mbathi, kwa kupigia debe kundi la ndizi kinyume na sheria za maadili ya wafanyikazi wa umma. Inapanga kuwasilisha kesi zaidi mahakamani.

#### **4. Kuorodhesha ufisadi kama swala la haki za kibinadamu**

Tume ya kitaifa ya kutetea haki za kibinadamu imechangia pakubwa katika kuorodhesha ufisadi kama swala muhimu la haki za kibinadamu nchini. Awali ufisadi ulionekana tu kama uhalifu wa kiuchumi. Tume hii imedhihirisha kuwa ufisadi unavuja raslimali zinazonuia kuinua maisha.

Tume hii imesisitiza na kuhamasisha umma kuwa ufisadi unamaanisha uhaba wa dawa za kukabiliana na makali ya ukimwi, raslimali chache kukabiliana na utovu wa usalama, ukosefu wa hazina ya masomo kwa watoto kutoka familia maskini.

Tume hii imehakikisha wakenya wanafahamu kuwa madhara ya ufisadi nipamoja na wakenya maskini kutoafikia haki zao muhimu.

Tume hii imeweza kuwasilisha ujumbe huo kupitia njia na mikakati mbalimbali kama vile jarida la *'Nguzo za Haki'* linaloelezea uhusiano kati ya ufisadi na haki za kibinadamu.

Tume hii pia inashawishi Tume nyengine za kitaifa za kutetea haki za kibinadamu barani Afrika kushughulikia ufisadi kama swala la haki za kibinadamu.

Azimio la Nairobi lililotolewa mnamo Machi 2006, wakati wa kufungwa kwa kongamano la bara la Afrika kuhusu haki za kibinadamu lililoandaliwa na Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu nchini lilikubaliana kwa kauli moja kuwa ufisadi una athari kubwa katika kuafikia haki za kibinadamu. Azimio la Nairobi lilitajwa katika kongamano lingine la haki za kibinadamu barani Afrika lililoandaliwa na Umoja wa Afrika kule Gambia mnamo Juni 2006. Aidha, azimio hilo la Nairobi lilipokelewa vyema wakati wa Tume za kitaifa za kuteteta haki za kibinadamu lililoandaliwa huko Geneva, Uswizi mnamo Aprili mwaka 2006.

Tume ya kitaifa ya kutetea haki za kibinadamu imetumia vyombo vya habari na vikao mbali mbali kuzungumza mara kwa mara dhidi ya ufisadi.

## **5. Utoaji wa huduma za kisheria kuhusiana na ukiukaji wa haki za kibinadamu**

Mnamo mwaka 2006, Tume hii ilianza kusikiza mfululizo wa kesi za ukiukaji wa haki za kibinadamu zilizoripotiwa kwa mahakama yake maalum.

Tume hii ina uwezo wa kuandaa kikao maalum cha mahakama na kutoa huduma za kisheria kwa waathiriwa wa ukiukaji wa haki za kibinadamu na hata kuwafidia. Wakati wa kipindi cha kati ya mwezi Januari na Machi mwaka 2006 walalamishi 460 wa haki za kibinadamu walifika kwayo, ilipokea barua 185 za kulalamikia ukiukaji wa haki za kibinadamu na barua pepe 32 pia za malalamishi kama hayo.

Kwa kuwasaidia wahasiriwa wa ukiukaji wa haki za kibinadamu, Tume hii imekuwa na athari ya moja kwa moja kwa maisha ya mamia ya wakenya. Idadi kubwa ya malalamiko yalowasilishwa katika Tume hii ni ishara tosha ya hamasisho na imani kubwa walo nayo Wakenya kwa Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu. Tume hii ilitekeleza uchunguzi kadhaa na kuchukua hatua za dharura.

## **6. Kuimarisha mshikamano katika mfumo wa utekelezaji wa sheria za jinai**

Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu inashawishi washiriki katika idara ya utekelezaji wa sheria za jinai kushirikiana kwa ajili ya haki kutendeka. Katika mkutano wa kitaifa wa majaji na mahakimu na washikadau wengine katika sekta hiyo uliofanyika mnamo juni mwaka 2006 na kuhudhuriwa pakubwa, ilipendekezwa pawe na mfumo ambapo maafisa wa idara hiyo katika nyanja kitaifa wanaweza kushirikiana mara kwa mara na wenzao wa nyanjani.

Aidha mapendekezo ya kubuniwa kwa kamati za mahakama yaliidhinishwa. Ushirikiano wa mashinani wa mashirika ya kisheria umeshuhudiwa katika maeneo ya Nakuru, Kericho na Meru. Warsha hiyo ya Juni mwaka 2006 ilifanyika kuboresha uhusiano wa watekelezaji wa sheria za jinai ili kuimarisha utoaji huduma za haki.

Ingawa polisi, idara ya mahakama, magereza na maafisa wa mahakama ni nguzo muhimu katika utekelezaji wa haki utendaji duni katika mojawepo ya idara hizo unaweza kuathiri nyengine. Mara nyingi hamna ushirikiano kati ya idara hizi hasa katika utungaji sera. Idara ya mahakama hasa hasa ndiyo inayoathirika kutokana na nyufa kwenye mfumo wa utekelezaji sheria za jinai. Utovu wa mashauriano katika mfumo huo umesababisha msongamno katika magereza. Uwajibikaji katika idara ya mahakama ni muhimu sana.

## **7. Utambuzi wa haki za kibinadamu katika mipango au utaratibu wa maendeleo**

Tume ya kitaifa ya kutetea haki za kibinadamu imechangia kuhakikisha kuwepo mtazamo kuwa haki za kibinadamu ni kigezo cha maendeleo miongoni mwa wafanyikazi wa serikali.

Mchango wa Tume hii umetambulika katika toleo linalotarajiwa la kwa kichwa; *'The development dimension: Integrating human rights into development'*, linalochapishwa na Organization on Economic Cooperate for Development (OECD).

Mtazamo huo unasisitiza haki ya kibinadamu ya kushiriki, usawa, kutobaguliwa, uwazi na uwajibikaji uwe sehemu ya mfumo wa maendeleo, hii ikiwemo ujenzi wa barabara na visima vya maji.

Mtazamo huo unatokana na mafunzo ambayo Tume hii imetoa kwa wafanyikazi wa umma katika wizara za kilimo, afya, barabara na ujenzi, leba na nyingine.

Katika kongamano la kitaifa kuhusu mtazamo wa haki za kibinadamu katika maendeleo, uliofanyika mwaka 2006 kwa ushirikiano na mashirika ya maendeleo kama vile SIDA Kenya, GTZ, CIDA Kenya na mashirika mengine, Wizara ya Mipango ya Kitaifa ilitambua haja ya kuidhinisha mtazamo wa haki za kibinadamu katika mfumo wa wastani wa matumizi ya pesa za serikali pamoja mageuzi katika matumizi ya pesa za umma.

Wizara ya Sheria na Maswala ya Katiba imetambua kuwa pana haja ya kuhamasisha maafisa wa bajeti na watunga sera kuhusu haja ya kuzingatia mtazamo wa haki za kibinadamu wanapotekeleza wajibu wao.

## **8. Kuwatia motisha wakereketwa wa kutetea haki za kibinadamu kupitia tuzo za kitaifa**

Tuzo za kitaifa za haki za kibinadamu na demokrasia zinazotolewa kila mwaka zinaheshimiwa na kutambuliwa sana. Kwa kutolewa na shirika la umma tuzo hizi zinahimiza watu binafsi na mashirika kupigania haki za kibinadamu na maongozi bora.

Mnamo Februari 2006, Tume iliandaa hafla yake ya tatu ya mwaka ya kutoa Tuzo kuhusu Demokrasia na Haki za kibinadamu. Tuzo la mafanikio maishani la 'Milele' lilimwendea marehemu Kasisi John Anthony Kaiser kwa kujitolea kwake maishani katika kutetea haki za kibinadamu humu nchini na pia akatuzwa Prof. Wangari Maathai kwa kazi yake ya kulinda mazingira na kuwapa uwezo kina mama.

Tuzo la Firimbi, la Mfichuzi wa kashfa lilimwendea John Githongo kwa ukakamavu wake kufichua kashfa ya Anglo-leasing iliyopelekea kujiuzulu kwa mawaziri kadhaa waliotajwa katika taarifa yake. Naye Davinder Lamba akatuzwa kwa kampeini yake ya 'Operation Firimbi' iliyofichua kashfa za unyakuzi wa ardhi na ufisadi humu nchini. Tuzo la 'Waziri' na la Polisi la 'Utumishi' (Police Station Award) hazikupeanwa kwani hakuna waziri yeyote ama kituo chochote cha polisi kilichostahili kupewa tuzo hilo.

## **9. Kuimarishwa na kulindwa kwa haki za kiuchumi, kijamii na kijinsia**

Tume hii imechangia katika kuimarika kwa kiwango cha haki za kiuchumi na kijamii. Ripoti yake kwa kichwa; *'The State of Human Rights 2003-4'*, ilitokana na tathmini iliyolenga yaloafikiwa katika nyanja ya haki za kiuchumi na kijamii nchini kenya. Ripoti za awali za haki za kibinadamu zililenga tu haki za raia na kisiasa.

Tume ya Kitaifa ya Kutetea Haki za Kibinadamu imefanikiwa kuanzisha mradi ambapo inatumia mfumo wa tamaduni kuhakikisha kuwa wajane waliopoteza mali yao kwa jamaa zao kufuatia kufariki kwa waume zao wanapata mali hiyo. Mradi huo ulianzishwa Mkoani Nyanza. Takriban wajane 30 na watoto wao wamenufaika. Mradi huo unatetea wajane kurithi mali kupitia mfumo huo wa tamaduni ambao unaheshimika kuliko sheria za kawaida. Tume ilipata usaidizi kutoka kwa mashirika ya kijamii, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wabunge wa eneo hilo.

Harakati kama hizo zilipongezwa na kutajwa kuwa mfano mzuri na shirika la Umoja wa Mataifa la kukabiliana na Ukimwi (UNAIDS) kwa kushughulikia masuala ya haki ya umiliki wa mali kwa kina mama kuhusiana na ugonjwa hatari wa Ukimwi, masuala ya ardhi, ajira na mazingira katika wilaya ya Malindi.

Mnamo 2005, Tume hii ilifanya uchunguzi wake wa kwanza wa umma huko Malindi mkoani Pwani. Uchunguzi huo ulifanywa kutokana na madai ya kukiukwa kwa haki za wafanyikazi na kuharibiwa kwa mazingira katika eneo la Marereni kutokana na shughuli za machimbo ya chumvi. Katika utathmini wake wa kibinafsi Tume hii ilifanya uchunguzi na kuwahamasisha wakazi wa sehemu hiyo kuhusu haki za kibinadamu na kutoa mwelekeo wa kulindwa kwa haki za wafanyikazi, ikiwa ni pamoja na wafanyikazi kupewa vifaa vya kuwalinda dhidi ya madhara wanapokuwa kazini.

Katika taarifa yake, Tume hii ilitoa mapendekezo yafuatayo:

- ↪ Kwamba kampuni za kutoa bidhaa ya chumvi ambazo zimekiuka masharti zichukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.
- ↪ kwamba kampuni za machimbo ya chumvi zinapasa kuhakikisha kwamba zinatoa vifaa kwa wafanyikazi kujikinga na hatari na kutowakata fedha za kugharamia vifaa hivyo katika malipo yao.
- ↪ Kampuni za machimbo ya chumvi zinahitajika kutoa vifaa vya kudumisha usafi kwa wafanyikazi wake wa kike na wa kiume.

## **10 Tume hii imetambuliwa na kuwajibika zaidi katika utumishi wa umma**

Hadi siku za hivi majuzi, Tume hii imekuwa ikichukuliwa kuwa ni shirika lisilokuwa la kiserikali na watumishi wa umma, vyombo vya habari na wakinzani wake. Lakini jambo hilo limeanza kubadilika. Taarifa za vyombo vya habari kuhusu Tume hii, zimethibitisha kwamba ni taasisi ya umma. Na kutokana na ukweli huo asasi zingine za umma zimejitokeza kupata ushauri.

Tume hii kwa mfano imepokea maombi ya kuitaka itoe mafunzo na ushauri kutoka kwa Idara ya Polisi, Idara ya Magereza Idara ya Upelelezi wa jinai, Idara ya Mawasiliano kwa Umma pamoja na wizara mbalimbali. Zaidi ya maafisa 1000 wa umma wamepokea mafunzo pia kutoka kwa Tume hii.

Tofauti ya majukumu kati ya Tume hii ya kitaifa na makundi ya umma yanayoshughulikia utetezi wa haki za kibinadamu iko wazi. Baada ya mashauriano kadhaa Tume hii ilikubaliana na mtandao wa kutetea haki za kibinadamu (K-HURINET) kuhusu msingi wa ushirikiano.

## **11. Tume hii imeanzisha mfumo wa kuwasilisha muundo wa mamlaka yake**

Tuna ofisi kuu jijini Nairobi na ofisi la kieneo Wajir ambayo ilianzishwa mnamo mwezi tarehe 16 Juni 2006.

Mnamo 2006, Tume hii ilitoa fursa zaidi kwa umma kuifikia kupitia kuhamisha makao yake makuu jijini Nairobi kutoka jumba la NSSF hadi jumba la CVS lililoko barabara ya Lenana katika sehemu ya Kilimani ambako kuna nafasi kubwa zaidi. Kutokana na hatua hiyo shughuli za Tume hii zinafanyika kwa wepesi zaidi. Pia Tume imeweza kuajiri wafanyikazi zaidi na wanafunzi wanaopata ujuzi wa kazi ili kumudu utekelezaji wa majuku yake yote na kazi nyingi ilizonayo.

Kwa upande mwingine kwa kufungua ofisi huko Wajir, Tume hii imeanzisha harakati za kusambaza shughuli zake kote nchini na hivyo itafungua ofisi katika wilaya zingine humu nchini.

## **12. Tume hii imetambuliwa kimataifa kupitia kuwekwa katika kamati ya kimataifa ya ushirikishaji wa asasi za kutetea haki za kibinadamu**

Mnamo mwezi April 2005, Tume hii iliwekwa katika kamati hiyo ambayo makao yake makuu yako katika ofisi za Balozi wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia haki za kibinadamu huko Geneva, Uswizi.

Asasi hizo ambazo ziko huru na ambazo zilibuniwa kupitia mikataba ya kimataifa kuhusu haki za kibinadamu ndizo ambazo hutambuliwa kimataifa. Mfumo wa uteuzi ulifanywa kwa utaratibu wake maalumu kupitia rais na Bunge baada ya arifa kutolewa kwa umma.

Na kutokana na kutambuliwa kimataifa, Tume hii imepata uwezo wa kuwa makao makuu ya asasi za Afrika zinazoshughulikia masuala ya haki za kibinadamu jijini Nairobi.

# CHANGAMOTO ZETU MUHIMU:

## 1. Udhamini na uhuru wa kifedha

Ruzuku inayopokewa na Tume hii kutoka kwa serikali haitoshi ikilinganishwa na kiwango kinachopewa Tume zingine kama vile Tume ya Uchaguzi (ECK) na Tume ya kukabiliana na Ufisadi KACC ambazo hupokea Bajeti ya shilingi bilioni tatu na bilioni 1.2 mtawalia.

Katika kipindi cha 2004/5, Tume hii ilipokea shilingi milioni 80 pekee licha ya kuwasilisha bajeti ya shilingi milioni 174, na kupokea kiwango cha shilingi milioni 90 katika Bajeti ya 2005/6.

Tume hutumia fedha hizo kutoka serikalini kuwaajiri na kuwalipa wafanyikazi na pia kugharamia mahitaji yake mengine mengi. Kutokana na upungufu huo wa fedha Tume imeshindwa kuwaajiri wafanyikazi wa kutosha na kufungua ofisi zaidi katika sehemu za mashambani ambapo ilikusudiwa kufunguliwa ofisi moja kila mwaka lakini mpaka sasa imeweza kufungua ofisi moja tu huko Wajir.

Changamoto kubwa ni kwamba Tume haina udhibiti kamili wa fedha zake. Ruzuku inayopata hupitia Wizara ya Sheria na Masuala ya Katiba. Jambo hilo linakwamisha uhuru wake kwa kuwa Wizara yenyewe ni moja ya asasi ambazo Tume hii inaweza kuitwa kuifanyia uchunguzi.

Tume imeendelea kuihimiza serikali lakini haijafanikiwa kukubali kuitengea fedha zake moja kwa moja. Jambo hilo limefanyiwa Tume ya kitaifa ya kukabiliana na ufisadi na hakuna sababu kwamba haliwezi kutekelezwa kwa ajili ya Tume hii.

## 2. Wafanyikazi

Kufikia mwezi Juni 2006, Tume ilikuwa na wafanyikazi 39, wakiwemo makamishna, huku ikiwa haijafikia kiwango kilichokusudiwa cha wafanyikazi 156 katika mpango wake wa kimsingi wa miaka mitano. Hata hivyo wafanyikazi iliyohitaji kuwa nao katika kipindi cha miaka tatu ni 94. Upungufu wa wafanyikazi umeathiri pakubwa uwezo wa Tume hii wa kutekeleza kikamilifu majukumu yake huku kukiwa na kazi nyingi ambazo hazijatekelezwa.

## 3. Ushirikiano na Serikali

Ili Tume iweze kufanya kazi kikamilifu, inahitaji ushirikiano mzuri zaidi kati yake na wizara na idara za serikali. Ingawa hilo limekuwa likihimizwa, ushirikiano huo haujaimarika kwa kiwango kinachohitajika.

Viongozi hasa katika Idara ya Polisi hawajaonyesha kutilia maanani Tume hii, ambapo bado haipewi ruhusa ya kuingia katika vituo kadhaa vya polisi kinyume na sheria na maongozi ya serikali. Katika taarifa ya wizara iliyowasilishwa Bungeni mnamo 2005, serikali kupitia Waziri katika Ofisi ya Rais alitoa mamlaka kwa Tume hii kuweza kuruhusiwa kuingia katika vituo vya polisi. Alisema wazi kwamba hakuna ruhusa kwa mtu yeyote kuitatiza Tume hii kuhusiana na suala hilo ambalo msingi wake uliwekwa kisheria.

Aliagiza kwamba arifa isambazwe kwa wahusika wote wa utekelezaji wa sheria endapo ingekuwa kuna baadhi yao ambao hawaelewi umuhimu huo. Ni jambo la kutia moyo kwamba idadi kubwa ya maafisa wa polisi katika vituo vingi humu nchini wamekuwa wakidumisha ushirikiano huo.

#### 4. Jinsi Tume inavyowasilwa kupitia maeneo ya mikoa

Tume hii sasa ina ofisi moja jijini Nairobi na ofisi mpya ya kieneo huko Wajir. Bado haiwezi kuwasiliwa kirahisi katika maeneo mengine ya nchi kama inavyoonyeshwa hapa chini.

| Mkoa                | Idadi ya watu waliowasilisha malalaamiko | Asilimia |
|---------------------|--|----------|
| Nairobi             | 581                                      | 41       |
| Kati                | 340                                      | 24       |
| Mashariki           | 154                                      | 11       |
| Rift valley         | 119                                      | 8        |
| Pwani               | 79                                       | 6        |
| Magharibi           | 70                                       | 5        |
| Nyanza              | 41                                       | 3        |
| Kaskazini Mashariki | 28                                       | 2        |
| Jumla               | 1,412                                    | 100      |

*Malalamiko yaliyopokelewa kwenye Tume katika kipindi cha 2004/5*

#### 5. Uhusiano na Bunge na Wizara ya Sheria na Masuala ya Katiba

Ili iweze kutekeleza kazi yake kikamilifu, Tume hii inahitaji uhusiano imara na Bunge ambalo ndilo linalohusika na sera, sheria za nchi na uwajibikaji wa umma. Uhusiano huo na Bunge haujakuwa imara. Tume haijapata fursa ya kushauriana kwa kina na kamati ya Bunge kuhusu utekelezaji wa

masuala ya kisheria ambayo ndiyo inayohusika na Haki za kibinadamu na masuala ya kisheria. Uhusiano na Wizara ya Sheria na Masuala ya Katiba umeimarika sana tangu kuteuliwa kwa waziri mpya katika wizara hiyo Mheshimiwa Martha Karua.

## **TUAMULIE WEWE**


Hakutaweza kuwa na uwajibikaji katika usimamizi wa asasi za umma kama wananchi hawatapewa fursa ya kujua kinachotekelezwa na asasi hizo kwa niaba yao na pia kupewa fursa ya kutoa michango yao. Na hizi ndizo zimekuwa juhudi zetu tokea mwanzo kutoa uhasibu wa umma na sasa tutafurahia sana kusikia maoni yako kuhusiana na jambo hilo na pia kutupatia mchango wako kuhusiana na kazi yetu.

Tafadhali tuma maoni yako kuhusu kazi yetu kwa  
Bi. Linda Ochiel

Nambari ya simu: 020-2717928/08/00

Barua pepe: [lochiel@knchr.org](mailto:lochiel@knchr.org)

ama kwa anwani yetu: S.L.P. 74359 - 00200, Nairobi, Kenya



**Maina Kiai**  
**Mwenyekiti wa Tume**

**28 Julai 2006**



**Mburu Gitu**  
**Katibu wa Tume**

